

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA - MIKINDANI



TAARIFA KWA UMMA.

MLIPUKO WA UGONJWA WA SURUA NA RUBELLA.

21 Februari 2023, **Mtwara**.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani COL. Emanuel Mwaigobeko anapenda kuutarifu umma kuwa kumetokea mlipuko wa ugonjwa wa **Surua na Rubella** ambapo wagonjwa **sita** wa surua na wagonjwa **nane** wa Rubella wamebainika kuwa na vimelea vya magonjwa hayo ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani.

Kutokana na uwepo wa mlipuko huo, Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani imeanza kutoa huduma ya chanjo ya **Surua na Rubella** kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano ambao hawakuwahi kupata au kukamilisha chanjo hiyo.

Hivyo basi wazazi na walezi wanatakiwa kuwapeleka watoto kwenye vituo vya kutolea huduma za chanjo vilivyopo karibu (zahanati na vituo vya afya) ili wakapate chanjo hiyo

Hata hivyo ugonjwa wa **Surua** unaweza kumpata mtu yelete, ukiona dalili za uwepo wa vipele vidogo vinavyoambatana na homa kali wahi kituo cha afya ili uweze kupata matibabu.

“Surua inaua, mpatie mtoto chanjo uokoe maisha yake”.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Jamadi A. Omari".

Jamadi A. Omari

Mkuu wa Kitengo Cha Mawasiliano Serikalini

Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA - MIKINDANI

